# JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO

## MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA

Imeandaliwa na:
Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa,
S. L. P. 166,
**MOROGORO**

Simu/Nukushi: +255 23 261 4727
**Barua pepe: info@morogoromc.go.tz**
**Tovuti: www.morogoromc.go.tz**



2025–2030

**DIBAJI**

Mkataba wa huduma kwa mteja ni ahadi ya kimaandishi kati ya Halmashauri ambayo ni mtoa huduma na wateja ambao ni wapokea hud uma zinazotolewa na Halmashauri, viwango vya huduma, majukumu na wajibu wa mteja na Halmashauri katika utoaji wa huduma. Pia Mkataba huu unaelezea namna ambavyo wateja watatoa mrejesho ikiwa ni pamoja na namna ambayo wateja watatoa malalamiko iwapo hawataridhika na huduma zinazotolewa.

Inategemewa kwamba, kupitia matumizi ya Mkataba huu, Halmashauri itawahusisha zaidi wateja wake katika kujieleza na kutoa maoni na mahitaji yao kuhusu huduma kulingana na matarajio yao. Kwa kufanya hivyo, Halmashauri itaweza kutoa huduma bora zaidi.

Ili Mkataba huu ufanye kazi kwa ufanisi, inabidi Mkataba huu uwe hati hai inayotokana na mahusiano mazuri ya kikazi tunayotarajia kuyajenga kati yetu sisi Watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na Wateja wetu. Ni matumaini yetu kuwa, Mkataba huu utasaidia kukuza uelewa wa haki na wajibu wa wateja wetu kuhusu upatikanaji wa ubora wa huduma zitolewazo na Halmashauri. Mkataba pia utawasaidia wateja katika kudai haki zao, kufahamu huduma zetu, viwango vya huduma na matarajio yao kwetu.

........................................
*Emmanuel J. Mkongo*
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**MOROGORO**

MKURUGENZI WA MANISPAA
MOROGORO

## 1. DIRA
Kuwa na jamii iliyo na maisha bora na endelevu yenye huduma bora za kijamii na kiuchumi ifikapo mwaka 2030.

## 2. DHIMA
Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wake itajitahidi kutoa huduma bora za kijamii na kiuchumi kwa kutumia vyema rasilimali zilizopo kwa manufaa ya wakazi wa Halmashauri na hata nje ya mipaka yake.

## 3. MAADILI
Katika kutoa huduma kwa wateja watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro tumedhamiria kufanya kilicho sahihi kwa kuzingatia maadili ya Msingi yafuatayo:-

- Kutoa huduma bora kwa wafanyakazi ya kuwahudumia wateja wetu kwa juhudi maarifa, kasi na kwa usahihi.

- Kufanya kazi kwa uadilifu kwa kuwa wasikivu, wakweli, wabunifu, waaminifu na kujituma katika matendo yetu.

- Kutoa huduma bila upendeleo kwa kuwatendea haki watu wote wakati wa kuwahudumia bila kujali hadhi, jinsia, dini, umri, ulemavu au ukabila.

- Matumizi sahihi ya taarifa kwa kutumia taarifa za kazi ipasavyo na kuwa makini na nyaraka na kumbukumbu za siri.

- Kutunza na kutumia ipasavyo dhamana tuliyopewa na kutambuliwa kutokana na matendo yaliyo sahihi.

- Kuwa watii kwa kuthamini na kuonyesha unyenyekevu kwa nchi yetu, mwajiri wetu watumishi wenzetu na Raia wenzetu. Kuwajibika kwa kuchukua dhamana ya matendo yetu kwa yale tuliyoyatenda ipasavyo au yale ambayo hatukuyatenda ipasavyo

- Kuwa na heshima kwa kuthamini haki na hadhi ya watu wengine.

- Kuzingatia muda wa huduma zinazotolewa kwa usahihi na uangalifu.

## 4. MADHUMUNI YA MKATABA

Madhumuni ya Mkataba huu wa huduma kwa mteja ni kukuza uelewa na upatikanaji wa ubora wa huduma zitolewazo na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwani huko nyuma tulikuwa tunatoa huduma lakini yawezekana wateja na wadau wetu hawakuwa wakizielewa vyema.

Hapo awali mtazamo wa Halmashauri ulikuwa ni matumizi ya kanuni na taratibu zinazoongoza utoaji wa huduma. Mtazamo wa sasa wa Halmashauri ni kupanga hatua za kuleta mabadiliko ya mtindo katika kuendesha shughuli za Halmashauri katika kutoa huduma. Mitizamo ya kisasa ya uendeshaji inayosisitiza kukubali, kubadilika, kutatua matatizo na kuwa na ushirikiano kati ya Halmashauri na asasi za kiraia, Wizara, Idara zinazotegemea na Wakala wa Serikali na watoa huduma wengine ili kuhakikisha huduma zetu ni rahisi katika upatikanaji wake zenye nafuu na zilizo katika kiwango cha juu cha ubora.

Mkataba huu utawasaidia wananchi kuelewa huduma zetu, viwango vya utoaji wa huduma hizo, namna ya kutupata na jinsi ya kushughulikia malalamiko yao kulingana na jinsi tunavyotoa huduma hizi.

## 5. WATEJA WETU

Wateja wetu wanaohudumiwa na Halmashauri yetu wamegawanyika katika makundi yafuatayo:-

- Wafanyabiashara
- Wazabuni
- Wanafunzi
- Wakulima
- Wafanyakazi
- Wafugaji
- Wanataaluma
- Wagonjwa
- Mamlaka za Serikali kuu
- Mamlaka za Serikali za Mitaa
- Watoa huduma wengine
- Wavuvi
- Wachimba Madini
- Mashirika yasiyokuwa ya Serikali (NGO's)
- Mashirika ya Taasisi za Kidini (FBO's)
- Vyama/Taasisi za Kijamii (CBO's)
- Taasisi za Kifedha
- Mashirika ya wahisani
- Vyama vya Siasa
- Jamii na washirika wengine wa Maendeleo.

**HUDUMA ZITOLEWAZO:**

- Kuajiri na kushughulikia maombi ya uhamisho wa Watumishi na kuratibu utoaji wa huduma.
- Kusimamia Taratibu, Kanuni, miongozo na Sheria katika kutoa huduma katika Jamii.
- Kuratibu masuala ya Utawala bora na mapambano dhidi ya Rushwa.
- Kukusanya mapato na kufanya malipo ya huduma na bidhaa.
- Kuendeleza na kuboresha Mipango Mjini, Maendeleo ya Ardhi, Kilimo/Mifugo mjini, Maliasili na Mazingira.
- Kusimamia ujenzi wa Miundo mbinu ya barabara, majengo, umeme na maji.
- Kuimarisha na kuendeleza shughuli za Biashara, Viwanda, masoko na sekta isiyo rasmi.
- Kuboresha maendeleo ya jamii, ustawi wa jamii na ushirika.
- Kuratibu uibuaji wa miradi, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
- Kutoa huduma za afya, tiba, afya kinga na kudhibiti taka ngumu na taka maji.
- Kutoa elimu ya msingi na Sekondari
- Kutoa ushauri wa kitaalam.
- Kusimamia utekelezaji wa Sheria za Nchi na Sheria ndogo za Halmashauri
- Kuratibu shughuli za burudani, michezo na maendeleo ya Vijana.
- Kuratibu mapambano dhidi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI.
- Kupokea malalamiko mbalimbali na kuyatatua.
- Kusimamia nidhamu na stahili kwa watumishi wote (watoa huduma) katika Taasisi yetu.

## WATEJA WA MANISPAA NA MATARAJIO YAO;

Wafuatao ni wateja wakuu wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na matarajio yao:

| MAJINA YA WATEJA/ WADAU | MATARAJIO KUTOKA MANISPAA |
|---|---|
| Watumishi wa Manispaa | ▢ Utawala bora<br>▢ Usalama kazini<br>▢ Ushirikiano na mwajiri<br>▢ Usawa katika kutoa na kupokea huduma<br>▢ Amani na utulivu<br>▢ Mazingira bora na mazuri ya kazi<br>▢ Fursa za kujiendeleza<br>▢ Kupata mshahara na maslahi mengine kwa wakati |
| Wananchi | ▢ Huduma bora za kijamii na kiuchumi<br>▢ Kushirikishwa katika shughuli zote za maendeleo na utoaji wa maamuzi<br>▢ Kutatuliwa kero zao<br>▢ Kupata taarifa za manispaa kuhusu miradi na maendeleo<br>▢ Kujua mapato na matumizi ya Manispaa |
| Sekretarieti ya Mkoa, OWM | ▢ Utoaji wa tafsiri sahihi wa sera, sheria na mikakati |
| TAMISEMI, Wizara, Idara zinazojitegemea n wakala wa serikali | • Shughuli mbalimbali pamoja na kuratibu na ufuatiliaji makini wa sera za kitaifa<br>• Uratibu wa utoaji taarifa za huduma zinazotolewa na Manispaa kwa wizara mbalimbali<br>▢ Kuwa kiungo kati ya Wizara za kisekta na Manispaa |
| Vyama vya Siasa | ▢ Kupokea taarifa za utekelezaji wa miradi<br>▢ Usawa bila kujali itikadi za kichama<br>▢ Tafsiri ya sera mbalimbali<br>▢ Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Utawala bora<br>▢ Ushirikishwaji katika mipango ya maendeleo |
| Madhehebu, vikundi na Taasisi za Dini, Asasi za Kiserikali na zisizo za Kiserikali na zisizo za Kiserikali, vyombo vya habari. Washirika na wahisani katika maendeleo | • Usawa bila kuzingatia itikadi za kiimani<br>• Ushauri wa Kitaalamu<br>• Kutambuliwa na kuthaminiwa kwa michango yao ya maendeleo<br>• Uhuru wa habari<br>• Matumizi mazuri ya fedha<br>Usimamizi mzuri wa miradi inayofadhiliwa na wadau wa maendeleo |
| Sekta binafsi | ▢ Mazingira bora ya biashara<br>▢ Amani na Utulivu<br>▢ Fursa sawa katika kufanya biashara<br>▢ Taarifa za masoko na takwimu za uchumi<br>▢ Ushirikishwaji katika kupanga mipango ya maendeleo |

| MAJINA YA WATEJA/ WADAU | MATARAJIO KUTOKA MANISPAA |
|---|---|
| CAG, PPRA, IAG | □ Utawala bora<br>□ Kujali thamani ya Fedha |
| Serikali kwa ujumla | □ Utawala bora<br>□ Amani na Utulivu<br>□ Kupata taarifa za utekelezaji wa mipango ya maendeleo kwa wakati<br>□ Kutekeleza sera, mipango pamoja na ilani ya uchaguzi ya chama Tawala |

**VIWANGO VYA UTOAJI HUDUMA**

**6. AHADI ZA IDARA KWA WATEJA NA WADAU WETU**

| DIVISHENI YA RASILIMALI WATU NA UTAWALA | | |
|---|---|---|
| **Na.** | **HUDUMA ZINAZOHUSIKA** | **VIWANGO VYA MUDA** |
| 1. | Kufikisha majalada kwa Maofisa wanaohusika na barua/dokezo | Ndani ya dakika 8 |
| 2 | Upatikanaji wa nyaraka na mafaili mbalimbali | Ndani ya dakika 8 |
| 3 | Kushughulikia barua zinazoingia na kutoka | Ndani ya siku 3 |
| 4 | Kushughulikia maslahi ya Watumishi, ruhusa kikazi na za kawaida | Ndani ya dakika 30 kwa kila mteja |
| 5 | Kusikiliza na kupokea malalamiko | Ndani ya dakika 30 kwa kila mteja |
| 6 | Kukamilisha ajira kwa Watumishi | Ndani ya siku 5 za kazi za wiki |
| 7 | Kutayarisha Mishahara ya Watumishi wapya, marekebisho ya mishahara, malimbikizo na kutuma menejimenti ya Utumishi wa Umma | Ndani ya siku 5 za kazi za ndani ya wiki |
| 8 | Kushughulikia mafao ya Wafanyakazi Wastaafu/uzazi | Ndani ya siku 2 za kazi za wiki |
| 9 | Kusimamia mahudhurio ya Watumishi | Kila siku |
| 10 | Kusimamia nidhamu ya Watumishi | Kila siku |
| 11 | Kusimamia raslimali za Manispaa | Kila siku |
| 12 | Kushughulikia barua zinazotoka(dispatching) baada ya taratibu za utawala kukamilika | Ndani ya dakika 10 |
| 13 | Kuhakikisha na kusimamia usafi na usalama wa Ofisi muda wote wa kazi | Kila siku |
| 14 | Kupokea simu | Ndani ya milio 3 |
| 15 | Kupokea wateja na kuwasikiliza | Ndani ya dakika 5 kila mteja |
| 16 | Kushughulikia mikopo ya Watumishi | Kila siku |

| DIVISHENI YA MIPANGO NA URATIBU | | |
|---|---|---|
| **Na.** | **HUDUMA ZINAZOHUSIKA** | **VIWANGO VYA MUDA** |
| 1. | Kuibua miradi kwa kushirikisha jamii (O&OD Review) | Ndani ya mwezi 1 miezi 3 kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha |
| 2. | Kutoa matangazo kwa wananchi juu ya miradi ya Manispaa itakayotekelezwa mwaka husika | Ndani ya siku 7 baada ya bajeti kupitshwa |
| 3. | Kupeleka fedha za miradi katika maeneo ya utekelezaji | Ndani ya siku 7 baada ya fedha kuingia |
| 4. | Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya Halmashauri ya Manispaa kila robo ya mwaka | Ndani ya siku 5 baada ya baada ya robo mwaka kuisha |
| 5. | Kukusanya takwimu kuhusu hali ya kiuchumi ya Halmashauri ya Manispaa | Ndani ya siku 90 kabla ya kuandaa bajeti |
| 6. | Kuratibu na kuandaa bajeti ya mwaka na kuiwakilisha kwa wadau mbalimbali wa Manispaa | Ndani ya miezi 3 (Januari-March) |
| 7. | Kuandaa mpango wa kazi na mtiririko wa matumizi ya fedha na kuiwakilisha mkoani | Ndani ya mwezi 1 |
| 8. | Kukagua miradi kwa kila robo ya mwaka na kamati ya mipango, uongozi na fedha | Ndani ya siku 5 kwa kila robo |
| 9. | Kukagua miradi kwa ajili ya malipo ya wakandarasi na kufuatilia matumizi ya fedha za serikali kulingana na miongozo iliyopo | Ndani ya siku 2 |
| 10. | Utoaji wa taarifa na tathmini za utekelezaji wa miradi | Kila mwezi |
| 11. | Kuandaa mabadiliko ya miradi | Ndani ya siku 15 tokea taratibu za kiutawala kukamilika |

| DIVISHENI YA AFYA, USTAWI WA JAMII NA HUDUMA ZA LISHE | | |
|---|---|---|
| **NA** | **HUDUMA ZINAZOTOLEWA** | **VIWANGO VYA MUDA** |
| 1. | Kutoa huduma ya dharula | Ndani ya dakika 15 toka dharula inapojitokeza |
| 2. | Wagonjwa wa kawaida kuonwa na daktari | Ndani ya saa 1 tokea mgonjwa kufika Hospitali |
| 3 | Ushauri nasaha na upimaji wa hiari | Ndani ya saa 1 toka mgonjwa kufika Hospitali |
| 4 | Huduma za kawaida za baabara (upimaji wa damu, widal, choo, mkojo, wingi wa damu) | Ndani ya saa 24 tokea mgonjwa kufika hospital |
| 5. | Utoaji wa dawa | Ndani ya dakika 15 |
| 6. | Huduma ya Afya ya uzazi na mtoto (PMTCT na ANC-Counceling) | Ndani ya saa 1 toka kufika tkwa mgonjwa |
| 7. | Kutoa huduma ya dharura baada ya masaa ya kazi | Ndani ya dakika 30 tokea dharula kujitokeza |
| 8 | Kupokelewa na kupata huduma na kuonwa na daktari | Ndani ya dakika 30 tokea kupokelewa |
| 9 | Daktari kuona wagonjwa clinic ya mpango wa Bima ya Afya | Ndani ya dakika 30 tokea kupokelewa |
| 10 | Kutafuta matatizo mengine ya wateja yanayohusu afya kwa ujumla | Ndani ya siku 5 tokea ombi kuwasilishwa |
| 11 | Kukusanya na kuandaa taarifa za Wagonjwa | Kila siku |
| 12 | Kutoa rufaa kwa wagojwa | Mara tu itakapothibitika imeshindikana katika kituo husika |
| 13 | Kufanya usajili wa Waganga wa jadi na Wakunga | Ndani ya miezi 3 tangu kupokelewa ombi |

| DIVISHENI YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI | | |
|---|---|---|
| **HUDUMA ZINAZOTOLEWA** | | **VIWANGO VYA MUDA** |
| 1. | Kutoa Elimu na ushauri kwa wafanya biashara | Kila siku |
| 2. | Kutoa leseni za biashara | Ndani ya siku 2 mara tu baada ya siku 21 za hiari kuisha |
| 3. | Kufanya ukaguzi wa leseni za biashara | Ndani ya miezi 2 mara tu baada ya siku 21 za hiari kuisha mwezi Julai |
| 4. | Kubuni vyanzo vipya vya Mapato | Miezi 3 kabla ya mwanzo wa mwaka wa fedha |

| DIVISHENI YA ELIMU YA AWALI NA ELIMU MSINGI | |
|---|---|
| **HUDUMA ZINAZOTOLEWA** | **VIWANGO VYA MUDA** |
| Kuidhinisha vibali vya uhamisho wa wanafunzi wa Elimu ya Msingi | Tutaidhinisha vibali vya uhamisho ndani ya siku 1 tangu kuwasilishwa ombi |
| Kusajili shule binafsi za awali na msingi | Tutasajili shule za awali na Msingi ndani ya siku 3 tangu kuwasilishwa kwa ombi |
| Kutoa idhini kwa wadau mbalimbali kuonyesha shughuli zao katika mashule | Tutatoa idhini ndani ya siku 2 tangu kuwasilishwa ombi |
| Kushughulikia misamaha ya karo kwa watoto yatima na kwa wenye wazazi wasiokuwa na uwezo | Tutashughulikia msamaha wa karo ya shule ndani ya siku sitini (60) tangu kuwasilishwa kwa ombi |
| Kushughulikia migogoro ya vyama, vilabu vya michezo, vikundi vya sanaa na vijana | Tutashughulikia mgogoro ndani ya siku thelathini (30) tangu kuwasilishwa taarifa ya mgogoro |
| Kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli za Halmashauri kwa umma kupitia vyombo vya habari | Tutatoa taarifa za utekelezaji kwa umma kupitia vyombo vya habari kila baada ya miezi mitatu (3) |

| DIVISHENI YA ELIMU SEKONDARI | |
|---|---|
| **HUDUMA ZINAZOHUSIKA** | **VIWANGO VYA MUDA** |
| Kuidhinisha vibali vya uhamisho wa wanafunzi wa Elimu ya Sekondari | Tutaidhinisha vibali vya uhamisho ndani ya siku 1 tangu kuwasilishwa ombi |
| Kusajili shule binafsi na Serikali za Sekondari zinazoanzishwa | Tutasajili shule za Sekondari ndani ya siku 3 tangu kuwasilishwa ombi |
| Kutoa idhini kwa wadau mbalimbali kuonyesha shughuli zao katika mashule | Tutatoa idhini ndani ya siku 2 tangu kuwasilishwa ombi |
| Kushughulikia misamaha ya karo kwa watoto yatima na kwa wenye wazazi wasiokuwa na uwezo | Tutashughulikia msamaha wa karo ya shule ndani ya siku sitini (60) tangu kuwasilishwa ombi |
| Kushughulikia migogoro ya vyama, vilabu vya michezo, vikundi vya sanaa na vijana | Tutashughulikia mgogoro ndani ya siku thelathini (30) tangu kuwasilishwa taarifa ya mgogoro |
| Kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli za Halmashauri kwa umma kupitia vyombo vya habari | Tutatoa taarifa za utekelezaji kwa umma kupitia vyombo vya habari kila baada ya miezi mitatu (3) |
| Kujibu barua za wateja zinazoingia Masjala ya Elimu | Kutoa majibu ya barua zinazoingia ndani ya siku 3 za kazi tangu kupokelewa barua. |

| DIVISHENI YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI | | |
|---|---|---|
| NA | HUDUMA ZINAZOHUSIKA | VIWANGO VYA MUDA |
| 1. | Kuibua na kuandaa mipango shirikishi ya maendeleo ya kilimo | Ndani ya siku 14 robo ya kwanza ya mwaka |
| 2. | Kutoa taarifa ya magonjwa ya mimea | Kila mwezi |
| 3. | Kutoa taarifa ya hali ya chakula ndani ya manispaa | Kila robo ya mwaka |
| 4. | Kusajili watoa huduma za kilimo, maduka ya kuuza | Ndani ya miezi 3 |
| 5. | Kusajili na kutoa vibali kwa mawakala wa pembejeo za kilimo | Ndani ya siku 14 |
| 6. | Kuandaa mashamba darasa na mashamba ya mfano kwa mazao ya chakula na biashara. | Kila mwaka |
| 7. | KUtoa taarifa ya masoko ya mazao | Kila mwezi |
| 8. | Kutoa taarifa ya hali ya hewa na chakula | Kila mwezi |
| 9. | Kufanya tathimini za hali ya chakula. | Kila robo Mwaka |
| 10. | Kushiriki katika udhibiti wa magonjwa/wadudu wa mimea/mazao. | Kila Mwezi |
| 11. | Kutoa takwimu na taarifa mbalimbali za kilimo. | Kila mwezi, robo na mwaka |
| 12. | Kutoa huduma za ugani kwa wakulima. | Kila siku |
| 13. | Kufanya tafiti mbalimbali za kilimo ikiwemo mimea/mazao, magonjwa na wadudu waharibifu. | Kila Mwaka |
| 14. | Kuibua na kusimamia miradi ya maendeleo ya kilimo. | Kila Mwaka |
| 15. | Kuratibu uundwaji wa vyama vya ushirika | Ndani ya siku 5 baada ya maombi kupokelewa |
| 16. | Kusajili vyama vya ushirika | Ndani ya siku 5 baada ya maombi kupokelewa |
| 17. | Kukagua na kutoa elimu kwa vyama vya ushirika | Ndani ya siku 15 kila baada ya robo mwaka |
| 18. | Kusaidia kuandaa sheria ndogondogo za ushirika | Ndani ya siku 30 kila inapojitokeza |
| 19. | Kushughulikia mashauri na migogoro ya vyama vya ushirika | Ndani ya mwezi 1 baada ya kupokea malalamiko |
| 20. | Kutoa tathimini na taarifa mbalimbali za maendeleo ya vyama vya ushirika | Ndani ya siku 15 kila baada ya robo Mwaka |

| DIVISHENI YA MIUNDOMBINU, UENDELEZAJI WA VIJIJI NA MIJI | | |
|---|---|---|
| **S/Na.** | **HUDUMA ZINAZOHUSIKA** | **VIWANGO VYA MUDA** |
| 1. | Kubadili matumizi ya ardhi | Tutatoa jibu la kukubaliwa au kukataliwa ombi la kubafili matumizi ya ardhi ndani ya siku tisini (90) tangu kuwasilisha ombi |
| 2. | Kukagua alama za mawe kabla ya umilikishaji wa ardhi | Tunakagua alama za mawe ndani ya siku kumi nne (14) tangu kuwasilishwa ombi |
| 3. | Kutengeneza ramani za hati (Dead Plan) | Tutatengeneza ramani za hati ndani ya siku thelathini tangu kuwasilishwa ombi. |
| 4. | Kuandaa rasimu ya hati (Title deed) | Tutaandaa rasimu ya hati ndani ya siku sitini (90) tangu kuwasilishwa ombi |
| 5. | Kukagua maendeleo na kupima ardhi | Tutafanya ukaguzi wa maeneo ya kupima ardhi ndani ya siku nne (4) tangu kuwasilishwa ombi. |
| 6. | Kupima ardhi/kiwanja | Tutapima ardhi/kiwanja ndani ya siku 30 tangu kulipia gharama za upimaji |
| 7. | Kukagua matumizi ya ardhi | Tutafanya ukaguzi wa matumisi ya ardhindnai ya siku tatu (3) za kazi tangu kuwasilihwa ombi |
| 8. | Kuandaa michoro mipya ya mipangomiji | Tutaanda mchoro mpya wa mipango miji ndani ya siku tisini (90) tangu kuwasilishwa kwa ombi |
| 9. | Kufanya utahamini majengo mapya | Tutatoa taarifa ya uthamini siku thelathini (30) tangu uthamini kufanyika |
| 10. | Kutoa vibali vya ujenzi | Ndani ya wiki tatu (3) tangu kuwasilisha maombi |
| 11. | Kupitia mapendekezo kwenye malaamiko ya malipo ya Wakandarasi | Ndani ya wiki tatu (3) tangu kuwasilisha maombi |
| 12. | Kukagua Miradi ya ujenzi inayofanywa na Halmashauri na kuhakiki ubora wake | Mradi unakaguliwa katika hatua zote ili kuhakiki ubora wake. |
| 13. | Kujenga Barabara kwa kushirikiana na TARURA | Kujenga Barabara yenye viwango kushirikiana na TARURA |
| 14. | Kutatua migogoro ya Ardhi | Migogoro inatatuliwa ndani ya Mwezi mmoja (1) |
| 15. | Kusimamia ukuaji wa Mji kwa kushirikaina na Ofisi ya Waziri wa Ardhi. | Mji unasimamiwa ipasanyo kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri wa Ardhi. |

| DIVISHENI YA MAENDELEO YA JAMII | | |
|---|---|---|
| **Na** | **HUDUMA ZINAZOHUSIKA** | **VIWANGO VYA MUDA** |
| 1 | Kupokea, kuhakiki na kushughulikia maombi ya mikopo | Ndani ya mwezi mmoja tokea kupokelewa kwa maombi |
| 2. | Kuandaa na kutoa mikopo kwa vikundi vya uchumi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu. | Ndani ya siku 5 za kazi |
| 3. | Kufanya vikao mbalimbali vya Idara | Kila jumatatu ya wiki, mwezi, robo, nusu na Mwaka |
| 4. | Kupokea na kushughulikia maombi ya usajili wa Vikundi/Asasi mbalimbali | Ndani ya siku 5 za wiki |
| 5. | Kuratibu uundwaji na usimamiaji wa vikundi vya Vijana, Wanawake, Watu wenye ulemavu na huduma ndogo za fedha | Muda wote wa kazi. |
| 6. | Kutoa elimu ya ujasiriamali na stadi za maisha kwa jamii | Muda wote wa kazi. |
| 7. | Kuratibu na kuhamasisha jamii kushiriki katika miradi ya Maendeleo | Muda wote wa kazi. |
| 8. | Kupokea na kusikiliza matatizo, migogoro na malalamiko ya Wanachi ndani ya jamii | Ndani ya siku 1 |
| 9. | Kutoa elimu kwa jamii kuhusu sera na miongozo ya jinsia, watu wanaoishi maeneo hatarishi ili wachukue tahadhari | Muda wote wa kazi. |
| 10 | Kutoa taarifa juu ya ustawi na Maendeleo ya jamii kila mwezi, robo, nusu na mwaka | Ndani ya siku 5 kwa kila kipindi husika |
| 11. | Kuratibu na kuunganisha wadau (NGO) wa Maendeleo katika kutoa huduma kwa jamii. | Ndani ya siku 5 za wiki |

| KITENGO CHA FEDHA NA UHASIBU | | |
|---|---|---|
| **Na.** | **HUDUMA ZINAZOHUSIKA** | **VIWANGO VYA MUDA** |
| 1. | Malipo ya hundi zilizoidhinishwa kulipwa na kumfikia mteja | Ndani ya siku 2 |
| 2. | Kutoa hundi kwa wateja na kuzisajili katika rejista kabla ya kuchukuliwa | Ndani ya dakika 5 kwa kila hundi |
| 3. | Kujibu hoja za mkaguzi wa ndani na wan je mara baada ya hoja kuibuliwa | Ndani ya siku 10 |
| 4. | Kuandaa "Recurent Budget" na kuiwakilisha sehemu husika | Ndani ya miezi 3(JanMarch) kabla ya mwaka wa fedha kuisha |
| 5. | Kuandaa na kufunga hesabu za mwisho wa mwaka kwa Idara zote za Manispaa | Ndani ya miezi 3 |
| 6. | Kuandaa taarifa za robo mwaka na kuzituma kwa RAS, TAMISEMI, na kuwasilisha katika vikao vya kisheria | Ndani ya siku 5 baada ya robo ya Mwaka kwisha |
| 7. | Kukusanya mapato | Tutaandaa hati za madai ya kodi ya huduma za Manispaa ila ifikapo Mwezi Machi, Juni Septemba na Desemba ya kila Mwaka |
| 8. | Tutafanya makadirio kwa kupiga hesabu ya 10% ya mauzo kwenye Nyumba za kulala wageni tarehe 1 – 5 ya kila Mwezi | Tutafanya makadirio kwa kupiga hesabu ya 10% ya mauzo kwenye nyumba za kulala wageni tarehe 1 – 5 ya kila Mwezi. |
| 9. | Tutaanda hati za madai ya kodi ya kupanga Viosk vya Manispaa tarehe 1 – 5 ya kila Mwezi | Tutaandaa hati za madai ya kodi ya kupanga Viosk vya Manispaa tarehe 1 – 5 ya kila Mwezi. |
| 10. | Ukusanya mapato ya vyanzo vyote vya mapato kila Mwezi | Kukusanya mapato ya vyanzo vyote vya mapato kila Mwezi. |
| 11. | Kulipa Wazabuni, watoa huduma wengina na madai ya Watumishi mbalimbali | Tutaandaa malipo ndani ya siku tatu (3) tangu kuwaislishwa hati ya madai. |

| KITENGO CHA MALIASILI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA | |
|---|---|
| **HUDUMA ZINAZOHUSIKA** | **VIWANGO VYA MUDA** |
| Kukagua, kuzoa na kusafirisha taka ngumu | Tutasafirisha taka ngumu kwenda dampo kila baada ya siku mbili (2). |
| Kutoa taarifa ya magonjwa ya mlipuko | Tutatoa taarifa ya magonjwa ya mlipuko kila siku endapo kuna mlipuko |

| KITENGO CHA MKAGUZI WA NDANI | | |
|---|---|---|
| NA | HUDUMA ITOLEWAYO KWA MTEJA | VIWANGO VYA MUDA |
| 1. | Kukagua na kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya Halmashauri kwa kutumia miongozo ya fedha | Ndani ya siku 5 kila baada ya robo Mwaka |
| 2. | Kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo ya Halmashauri ili kuona kama taratibu na thamani ya fedha(value for money) kama imezingatiwa | Ndani ya siku 1 |
| 3. | Kukagua mikataba ya wakandarasi kama taratibu za Fedha na nyaraka ambatanishwa kama zinakidhi kanuni na taratibu za fedha | Ndani ya siku 2 kila hitaji |
| 4. | Kukagua risiti za urejeshaji masurufu | Ndani ya siku 1 |
| 5. | Kuandaa majibu ya Audit Querries za Wakaguzi wa nje kila inapojitokeza | Ndani ya siku 10 |

| KITENGO CHA TEHAMA | | |
|---|---|---|
| NA | HUDUMA ZITOLEWAZO | VIWANGO VYA MUDA |
| 1. | Kupata ushauri na matumizi ya mifumo ya TEHAMA toka wakala wa serikali mtandao (eGA) | Ndani ya siku 15 tokea hitaji kuwasilishwa |
| 2. | Kutoa ushauri wa kitaalamu na kuandaa hadidu rejea za vifaa vya TeHAMA | Ndani ya siku 5 baada ya ombi kuwasilishwa |
| 3. | Kushughulikia matengenezo ya tovuti na kuhuisha(upadate) taarifa za tovuti ya Manispaa | Ndani ya siku 5 baada ya kupewa maagizo |
| 4. | Kusimamia usalama na uhifadhi wa vifaa vya TEHAMA | Kila siku |
| 5. | Kuhakikisha usalama, msaada wa kiufundi na upatikanaji wa mifumo ya TEHAMA kwa wateja | Kila siku |
| 6. | Kutoa taarifa juu ya uhuishaji wa tovuti, mawasiliano ya kimtandao(e-mails) na usalama wa vifaa vya TEHAMA | Kila sku |

| NA | HUDUMA ITOLEWAYO KWA MTEJA | VIWANGO VYA MUDA |
|---|---|---|
| 8. | Kukagua mali toka kwa Wazabuni na kuingiza katika vitabu vya mali (store ledger) | Ndani ya siku 7 |
| 9. | Kuandaa nyaraka muhimu za manunuzi kwa ajili ya malipo ya mzabuni | Ndani ya siku 1 |
| 10. | Kuandaa mpango na taarifa ya manunuzi kwenda CMT na PPRA | Ndani ya siku 20 |

| KITENGO CH A HUDUMA ZA SHERIA | | |
|---|---|---|
| **NA** | **HUDUMA ITOLEWAYO KWA MTEJA** | **VIWANGO VYA MUDA** |
| 1. | Kupitia mikataba ya kisheria inayohusu Halmashauri ya Manispaa | Ndani ya siku 5 baada ya kupokea mkataba |
| 2. | Kupitia katiba za vikundi vya jamii na kutoa ushauri | Ndani ya siku 5 baada ya kupokea mkataba |
| 3. | Kumhudumia mteja anaeingia mkataba na Manispaa au mgogoro na Manispaa | Ndani ya siku 1 |
| 4. | Kuandaa nyaraka za kuwasilisha mahakamani | Ndani ya siku 21 tokea shauri kufunguliwa |
| 5. | Kutoa elimu ya katiba na haki za binadamu kwa umma | Kila baada ya miezi 3 |
| 6. | Kujibu barua mbalimbali za wateja zinazohusu masuala ya kisheria | Kila siku |
| 7. | Kuandaa mabaraza ya kata na kusimamia utendaji kazi kwa kuwapa elimu | Ndani ya siku 15 kila hitaji linalojitokeza |
| 8. | Kuhakikisha kuna usalama katika kila kata ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro | Kila siku |

| KITENGO CHA UDHIBITI WA TAKA NA USAFISHAJI | |
|---|---|
| **HUDUMA** | **MATARAJIO** |
| Kusafisha masoko na stendi za mabasi makubwa na madogo | Kuingia Mikataba na Wazabuni wa kusafisha kila siku Masoko na stendi za mabasi makubwa na madogo kila Mwaka wa fedha. |
| Kusafisha barabara, mifereji na hifadhi za barabara | Kuingia mkataba na mzabuni wa kusafisha kila siku katika barabara, mifereji na hifadhi za barabara zenye shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii kila mwaka wa fedha |
| Kuzoa taka na kwenda kuzitupa Dampo | Kuzoa taka na kwenda kuzitupa Dampo kila siku |
| Kukusanya ada ya uzoaji wa taka | Kuingia Mikataba na Wazabuni wa kukusanya ada ya uzoaji wa taka kila Mwaka wa Fedha na ada kukusanya mwisho wa Mwezi baada ya Wananchi kupokea huduma |
| Kukusanya ada ya utupaji wa taka dampo | Kukusanya ada ya utupaji wa taka dampo kwa kutumia mashine ya POS kwa siku/mwezi/mwaka kwa kadiri ya mahitaji ya mteja |
| Uendeshaji wa shughuli za kila siku za Dampo | Kutumia mitambo ya Manispaa katika uendeshaji wa shughuli za kila siku za Dampo |
| Kukodisha magari ya kubeba taka ngumu | Kukodisha magari ya kubeba taka ngumu kwa tripu na kwa mwezi kwa kadiri ya mahitaji ya mteja |
| Kukodisha gari la kunyonya maji taka | Kukodisha gari la kunyonya maji taka kwa idadi ya tripu kwa kadiri ya mahitaji ya mteja |
| Kutoa elimu ya udhibiti wa taka na usafishaji wa taka kwa wananchi | Kutoa elimu ya udhibiti wa taka na usafishaji wa taka kwa wananchi mara moja kwa mwezi |
| Kutoza faini kwa wananchi wanavunja sheria za usafi kwa makusudi | Kutoza faini kwa Wananchi wanavunja Sheria za usafi kwa makusudi baada ya kupewa elimu na ilani |
| Kufanya ukaguzi wa shughuli za udhibiti wa taka na usafishaji | Kufanya ukaguzi wa shughuli za udhibiti wa taka na usafishaji kila siku kwa maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa taka na mara moja kwa wiki kwenye maeneo yenye uzalishaji mdogo wa taka. |

| KITENGO CHA MICHEZO, SANAA NA UTAMADUNI | | |
|---|---|---|
| **NA** | **HUDUMA ITOLEWAYO KWA MTEJA** | **VIWANGO VYA MUDA** |
| 1. | Kutoa vibali vya matangazo/promosheni | Ndani ya siku 1 |
| 2 | Kutoa vibali vya tiba asili | Ndani ya siku 1 |
| 3. | Kuratibu shughuli za usajili wa vikundi vya burudani na sanaa | Ndani ya siku 1 |
| 4. | Kuratibu shughuli za Mwenge wa Uhuru | Miezi 3 kabla ya ratiba ya Mwenge |
| 5. | Kuandaa mipango ya michezo ya UMITASHUMITA/UMISSETA | Mwezi 1 kabla ya michezo kuanza |
| 6. | Kufanya taratibu za usajili wa Vilabu na vyama | Ndani siku 1 |

## 7. WAJIBU, HAKI NA MAJUKUMU YA WATEJA KWA MANISPAA;

Pamoja na haki na wajibu walionao wateja kwa Manispaa, Mkataba huu wa huduma kwa mteja unawawezesha Wateja kuelewa ni huduma zipi zitolewazo na viwango vya ubora.

### *7.1.* Wajibu wa Wateja

Wateja wana jukumu la kufuata kanuni na taratibu zilizopo ili wasaidie manispaa kutoa huduma bora na kuhakikisha mahusiano mazuri yanakuwepo

- Kufuata sheria na taratibu za Manispaa
- Kushiriki kutekeleza sera, sheria, mipango ya maendeleo na maelekezo ya serikali
- Kutoa taarifa sahihi na za kweli na kwa wakati muafaka
- Kufanya kazi kwa bidii na maarifa kwa ajili ya maendeleo yamanispaa na Taifa kwa ujumla
- Kulinda mali na kutunza mazingira kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo
- Kuzingatia muda wa utoaji wa huduma
- Kuheshimu na kutiii mamlaka za manispaa
- Uwajibikaji wa wateja katika miradi mbalimbali ya maendeleo

### 7.2 Haki ya mteja

Kutokana na Mkataba huu pamoja na matarajio makubwa kutoka kwa wadau na wateja wa Manispaa, wao pia wanastahili kupata haki na stahili zifuatazo: -

- Haki ya kuheshimiwa
- Haki ya kupata huduma kwa kiwango na muda uliokubalika
- Haki ya kusikilizwa
- Haki ya kupata huduma kwa uwazi na usawa
- Haki ya kushirikishwa kwenye mapitio ya mkataba wa huduma kwa mteja
- Haki ya kupata taarifa na habari zinazohusiana na shughuli zao na za manispaa
- Haki ya kupata rufaa kuhusiana na uamuzi wa suala lolote linalomhusu
- Haki ya kutoa na kuwasilisha malalamiko kwa kufuata sheria, kanuni, taratibu na ngazi zilizowekwa
- Haki ya kushirikishwa kwenye mipango ya Maendeleo

## 8. MATARAJIO NA MATEGEMEO YA MANISPAA KUTOKA KWA WATEJA

Wateja wa Manispaa pamoja na haki zilizoainishwa kwa upande wake Manispaa inategemea kuwa na wateja wake watazingatia yafuatayo: -

- Maelewano na mahusiano mazuri
- Kuheshimu wataalamu n watumishi
- Kuepuka kashfa na majungu yanayolenga kuwakomoa watumishi
- Kuwa na taarifa sahhi za shughuli za watumishi
- Kuzingatia na kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa
- Kuepuka migongano na migogoro kati ya wateja na watumishi
- Kutumia masanduku ya maoni kutoa dukuduku zao
- Wateja kuzingatia na kufuata ngazi za uongozi kutoa malalamiko yao

## 9. MAONI NA TAARIFA ZA MREJESHO WA MKATABA

Ili kuboresha huduma zetu pamoja na uwajibikaji wa watumishi na Manispaa kwa ujumla manispaa yetu iko tayari kupokea, kukubali maoni na ushauri na kufanyia kazi kwa kuzingatia mambo yafuatayo: -

- Mapungufu yaliyomo katika utoaji huduma
- Malalamiko na mrejesho wa utendaji kazi
- Changamoto za wateja
- Kuboresha huduma na utendaji wa watumishi
- Kufanya kazi ushauri, maoni na malalamiko ya wateja

Manispaa kwa upande mwingine imedhamiria kuhakikisha Mkataba wake wa huduma kwa mteja ni wa kudumu, na hapana budi huduma zitakazotolewa zitakidhi matarajio na viwango vilivyokubalika. Ni matarajio yetu kwamba viashiria na ufanisi wa utoaji huduma na majukumu vyote vitapimwa kwa kuzingatia utekelezaji wa malengo ya kila Divisheni na Kitengo kama yalivyoainishwa ndani ya mpango mkakati wa Manispaa.

## 10. KUFANYA MAPITIO YA HUDUMA KWA MTEJA

Mkataba huu umeandaliwa na Manispaa kutokana na maoni, ushauri na changamoto kutoka kwa wateja na wadau, hivyo utafanyiwa mapitio kila baada ya miaka 3, au itakapobainika kuna upungufu au maoni na ushauri wa wateja ili kukidhi matarajio yao kutokana na mabadiliko mbalimbali.

Mapitio ya mkataba wa huduma kwa mteja yatawezesha manispaa, wadau, na wateja kufanikisha masuala muhimu kama vile kuwa na mkataba: -

- Hai na unaotekelezeka
- Unaokubaliwa na pande zote zinahusika
- Unaozingatia dhana shirikishi
- Unaozingatia mabadiliko na kwenda na wakati
- Unaowezesha kuboresha utoaji huduma
- Unaoweza kukabiliana na changamoto na mapungufu yanayojitokeza wakati wa utekelezaji wake

NB: Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro inaweza ikapata changamoto za kutofikia baadhi ya viwango vilivyokubalika kutokana na changamoto mbalimbali za wadau wa maendeleo

## 11. MAWASILIANO KWA PANDE ZOTE

Manispaa ina mawasiliano ya simu za mezani, barua pepe, nasanduku la barua kwa njia ya Posta ili kuwezesha mawasiliano ya HARAKA zaidi. Mawasiliano yote yatumwe kwa Mkurugenzi wa Manisipaa ya Morogoro. Anwani za mawasiliano zipo ukurasa wa mwisho.

*Ofisi ya Malalamiko*,
Mkurugenzi wa Manispaa,
S.L.P. 166,
**MOROGORO**

***Simu***: 023 2614727
***Tovuti***: www.morogoromc.go.tz
***Barua pepe***: info@morogoromc.go.tz